

HALMASHAURI YA WILAYA YA MKINGA



TANGAZO LA ZABUNI ZA MAPATO

KWA KIPINDI CHA 2017/2018

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga anawatangazia wafanya biashara wote Zabuni ya ukusanyaji wa mapato katika kipindi cha 2017-2018. Zabuni zinazotangazwa ni:-

ZABUNI NAMBA	MAELEZO YA ZABUNI
LGA/133/2017-2018/HQ/NC/01	Ushuru wa Samaki na dagaa maeneo yote ya Wilaya ya Mkinga
LGA/133/2017-2018/HQ/NC/02	Ushuru wa Mazao ya misitu maeneo yote ya Wilaya ya Mkinga
LGA/133/2017-2018/HQ/NC/03	Ushuru wa chumvi maeneo yote ya Wilaya ya Mkinga
LGA/133/2017-2018/HQ/NC/04	Ushuru wa mawe ya kawaida na urembo, mchanga, kokoto na kifusi
LGA/133/2017-2018/HQ/NC/05	Ushuru wa stendi ya kituo cha magari Maramba na stendi ya mabasi Manza
LGA/133/2017-2018/HQ/NC/06	Ushuru wa mazao isipokuwa Korosho na katani

MASHARTI YA WAOMBAJI:

- a) Mwombaji awe na leseni ya biashara ilio hai na inayofanana na biashara hiyo
- b) Mwombaji awe na Taxpayer Identification Number (TIN), power of Attorney
- c) Mwombaji awe na vitendea kazi vya kutosha kumudu vyema Zabuni aliyoomba
- d) Mwombaji asiwe anadaiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga au sehem yejote
- e) Mwombaji atamke wazi atakusanya kiasi gani cha chini (at least) kwa mwezi na asilimia ya gawio lake kwa mwezi
- f) Mkataba kwa kila zabuni utakuwa wa Miezi mitano mitano na utahuishwa tena kwa miezi mitano, pia mkataba wa jumla mwisho Juni 30,2018
- g) Mzabuni aliyeshinda zabuni katika Halmashauri ya Mkinga awali na akashindwa kutekeleza zabuni hiyo, maombi yake hayatafikiriwa
- h) Mwombaji aambatanishe uthibitisho wa utendaji kazi za kukusanya ushuru kutoka taasisi yeoye ya umma alizofanya kazi

- i) Mwombaji atakayeshinda atatakiwa kukusanya ushuru wote na kuwasilisha Halmashauri kisha atarudishiwa asilimia ya gawio lake kulingana na masharti yaliyomo katika zabuni na kuweka **dhamana ya miezi miwili** kwa kiwango alichosema anaweza kuwasilisha kwa mwezi kabla ya kusaini mkataba
- j) Kabrasha la Zabuni linapatikana ofisi ya Katibu wa Bodi ya Zabuni
- k) Kulipa ada ya maombi Tsh. 70,000/= kwa kila Zabuni. Fedha hizi hazitarejeshwa
- l) Barua za maombi zenyе maelezo ya kina na viambatanisho husika pamoja na maelezo ya mahali ofisi yake ilipo zitumwe kwa: KATIBU, BODI YA ZABUNI, S.L.P 6005 TANGA.
- m) Mwisho wa kupokea maombi ya Zabuni ni tarehe **18.08.2017** saa 04:00 Asubuhi na ufunguzi wa Zabuni utafanyika siku hiyo hiyo muda mfupi baadae katika ukumbi wa mikutano jengo la Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga. Waombaji wa Zabuni au wawakilishi wao wanakaribishwa katika ufunguzi huo.

RASHID K. GEMBE
MKURUGENZI MTENDAJI (W)
MKINGA